

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**MKUTANO WA SABA**

**YATOKANAYO NA KIKAO CHA HAMSINI NA MBILI**

**21 JUNI, 2017**

## **MKUTANO WA SABA**

### **KIKAO CHA HAMSINI NA MBILI TAREHE 21 JUNI, 2017**

#### **I. DUA:**

Dua ilisomwa saa 3:00 asubuhi na Mhe. Mussa A. Zungu (Mwenyekiti) na kukiongoza Kikao.

Makatibu mezani:

1. Ndg. Laurance Makigi
2. Ndg. Zainab Issa

#### **II. HATI ZA KWASILISHA MEZANI**

1. Naibu Waziri wa Fedha na Mipango aliwasilisha Mezani Maelezo ya Waziri wa Fedha na Mipango kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka, 2017 (*The Finance Bill, 2017*).
2. Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti aliwasilisha Mezani kwa niaba ya Mwenyekiti Maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka, 2017 (*The Finance Bill, 2017*).
3. Mhe. Cecil David Mwambe kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Fedha na Mipango aliwasilisha Mezani Maoni ya Msemaji huyo kuhusu Muswada wa Sheria wa Fedha wa Mwaka, 2017 (*The Finance Bill, 2017*).

#### **III. MASWALI**

Maswali yafuatayo yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kujibiwa na Serikali.

## **OFISI YA RAIS (TAMISEMI)**

Swali Na. 426: Mhe. Boniventura Destery Kiswaga

Nyongeza: Mhe. Boniventura Destery Kiswaga  
Mhe. David Ernest Silinde  
Mhe. Sebastian Simon Kapufi  
Mhe. George Malima Lubeleje  
Mhe. Kangi Alphaxard Lugola  
Mhe. Joseph Michael Mkundi

Swali Na. 427: Mhe. Almas Athuman Maige

Nyongeza: Mhe. Almas Athuman Maige  
Mhe. Yahaya Omary Massare  
Mhe. Sebastian Simon Kapufi  
Mhe. Cecil David Mwambe  
Mhe. Qambalo Willy Qulwi  
Mhe. Ally Seif Ungando  
Mhe. Julius Kalanga Laizer

Swali Na. 428: Mhe. Maria Ndila Kangoye

Nyongeza: Mhe. Maria Ndila Kangoye  
Mhe. Edward Franz Mwalongo  
Mhe. Cecilia David Paresso  
Mhe. Shally Joseph Raymond

Swali Na. 429: Mhe. Mendrad Lutengano Kigola

Nyongeza: Mhe. Mendrad Lutengano Kigola  
Mhe. Cosato David Chumi  
Mhe. Innocent Sebba Bilakwate  
Mhe. Venance Methusalah Mwamoto  
Mhe. Joyce John Mukya  
Mhe. Chacha Marwa Riyoba  
Mhe. Kasuku Samson Bilago

## **WIZARA YA MALIASILI NA UTALII**

Swali Na. 430: Mhe. Dkt. Immaculate Sware Semesi

Nyongeza: Mhe. Dkt. Immaculate Sware Semesi  
Mhe. Shaabani Omari Shekilindi  
Mhe. Zuberi Mohamedi Kuchauka

Swali Na. 431: Mhe. Naghenjwa Livingstone Kaboyoka

Nyongeza: Mhe. Naghenjwa Livingstone Kaboyoka  
Mhe. Suleiman Yussuf Ally  
Mhe. Rashid Abdallah Shangazi  
Mhe. Philip Augustino Mulugo  
Mhe. Issaya Zacharia Paulo

## **WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**

Swali Na. 432: Mhe. Juma Othman Hija

Nyongeza: Mhe. Juma Othman Hija  
Mhe. Susan Anselm Lyimo  
Mhe. Mgeni Jadi Kadika  
Mhe. Khadija Nassir Ali  
Mhe. Fredy Mwakibete Atupele  
Mhe. Oliver Daniel Semuguluka  
Mhe. Sevelina Silvanus Mwijage  
Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi

Swali Na. 433: Mhe. Jacqueline Ngonyani Msongozi

Nyongeza: Mhe. Jacqueline Ngonyani Msongozi  
Mhe. Issa Ali Mangungu  
Mhe. Raisa Abdallah Mussa  
Mhe. Amar Hussein Nassoro  
Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi  
Mhe. Devotha Mathew Minja

## **WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**

Swali Na. 434: Mhe. Juma Hamad Omar

Nyongeza: Mhe. Juma Hamad Omar  
Mhe. Daniel Nsanzugwako  
Mhe. Ritta Enespher Kabati  
Mhe. Jesca David Kishoa  
Mhe. Khatib Said Haji

## **WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Swali Na. 435: Mhe. Deogratias Francis Ngalawa

Nyongeza: Mhe. Deogratias Francis Ngalawa  
Mhe. Pauline Philipo Gekul  
Mhe. Josephine Johnson Genzabuke  
Mhe. Joseph Kasheku Musukuma  
Mhe. Abdallah Dadi Chikota  
Mhe. Joseph Leonard Haule  
Mhe. Seif Khamis Gulamali  
Mhe. Emmanuel Adamson Mwakasaka

## **WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI**

Swali Na. 436: Mhe. Omary Tebweta Mgumba

Nyongeza: Mhe. Omary Tebweta Mgumba

## **MATANGAZO**

Wageni mbalimbali walioko kwenye *Galleries* za Ukumbi wa Bunge walitambulishwa.

## **MWONGOZO WA SPIKA**

1. Mhe. Joseph Kasheku Musukuma aliomba Mwongozo chini ya Kanuni ya 68(7) kuhusu kupigwa Ng'ombe minada kwamba Waziri alitangaza kusitishwa kwa zoezi hilo. Tunaomba kauli ya Serikali kuzuia zoezi hilo.

Mwenyekiti aliiomba Serikali walifanyie ufumbuzi.

2. Mhe. Cecil David Mwambe aliomba Mwongozo chini ya Kanuni ya 47, katika Wilaya ya Masasi kuna tatizo kubwa la umeme na ahadi ya Rais wakati wa ziara yake ni mpaka tarehe 30 Mei, 2017 umeme utakuwa umewekwa.

Mwenyekiti, alimuelekeza Mhe. Cecil David Mwambe awasiliane na Waziri husika.

3. Mhe. Mch. Peter Simon Msigwa, Kura ya Bajeti inapigwa kwa ajili ya kupidisha matumizi na mapato ya Serikali kwa ajili ya kukusanya kodi na ni kura ya imani kwa Serikali. Je ni halali kusema fedha hazitofika Majimboni kwa Waheshimiwa Wabunge waliopiga kura ya hapana?

Mwenyekiti jambo lako limeshafanyiwa uamuzi.

4. Mhe. Abdallah Ally Mt Olea aliomba Mwongozo wa Spika chini ya Kanuni ya 47(1) na 47(3) kwamba upimaji wa majibu Muhimbili umekuwa *computerized* lakini changamoto ni kukatika kwa umeme jambo ambalo hupelekea vifo.

Mwenyekiti alimuelekeza Mhe. Abdallah Ally Mt Olea awasiliane na Waziri husika.

5. Mhe. Jesca David Kishoa aliomba Mwongozo wa Spika chini ya Kifungu 68(7) kwamba wakati wa kujibu swali Naibu Waziri wa Fedha alikanusha kwamba Tanzania haina viwango vya juu vya kodi.

Mwenyekiti alijibu Mwongozo huo kwamba hizo ndio taarifa sahihi za Serikali.

6. Mhe. Devotha Mathew Minja aliomba Mwongozo wa Spika chini ya Kanuni ya 68(7) na 46 kuwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto wakati wa kujibu swali lake la Nyongeza kwa swali 433. Kwanini Waziri anaacha kujibu swali moja kwa moja na kuleta Siasa.

Mwenyekiti alijibu Mwongozo huo kwamba Waziri kupongeza Mbunge ye yote si jambo baya.

7. Mhe. Constantine John Kanyasu aliomba Mwongozo wa Spika chini ya Kanuni ya 68(7) kuhusu Tatizo la Maji katika Mji wa Geita na visima vingi vimekauka, nini hatua za Serikali?

Mwenyekiti alimuelekeza Mhe. Constantine John Kanyasu aonane na Waziri anayehusika na maji.

8. Mhe. Mbarouk Salim Ali aliomba Mwongozo chini Kanuni ya 68(7), wakati Mhe. Harrison George Mwakyembe anajibu swali la Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi kuhusu watangazaji wa TBC kutoa taarifa za uongo na kuchukuliwa kuwa ni suala la kawaida.

Mwenyekiti alijibu Mwongozo huo kuwa hawa watu walishasamehewa na kesi yao ilishafungwa.

#### **IV. KUSITISHA BUNGE**

Shughuli za Bunge zilisitishwa saa 5:40 asubuhi hadi saa 10:00 jioni.

#### **V. SHUGHULI ZA BUNGE KUREJEA**

Shughuli za Bunge zilirejea saa 10:00 jioni ambapo Mwenyekiti wa Bunge alitoa Taarifa ya Mwenyekiti kwamba Bunge halitoweza kuendelea kwa kuujadili Muswada wa Fedha, 2017 kwa kuwa marekebisho yaliyopendekezwa na Kamati ya Bajeti kwa Muswada

huo yamekuwa mengi kiasi ambacho Muswada huo umelazimika kuchapwa upya.

## **VI. KUAHIRISHA SHUGHULI ZA BUNGE**

Shughuli za Bunge ziliahirishwa saa 10:05 jioni hadi kesho tarehe 22 Juni, 2017 saa 3:00 asubuhi.